**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA CHAMWINO, HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO, MKOA WA DODOMA NA MADIWANI KATIKA KATA 11 ZA TANZANIA BARA

**Dodoma, 25 Septemba, 2026**

1. Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Chamwino, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma. Nafasi hiyo imetokea baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumteua aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi wake ulifanyika tarehe 26 Agosti, 2026 na kuthibitishwa na Bunge tarehe 28 Agosti, 2026.
2. Aidha, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 57(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, tumepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuhusu uwepo wa nafasi wazi za madiwani 11 kwa Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zilitokana na vifo vya madiwani nane (08) kwa nyakati tofauti na madiwani watatu (03) kujiuzulu.

   Jimbo na kata zenye nafasi wazi zimeoneshwa katika Jedwali Na.1 na Na.2. kama ifuatavyo: -

**Jedwali Na. 1: Jimbo lenye Nafasi Wazi**

| Mkoa | Halmashauri | Jimbo |
|---|---|---|
| Dodoma | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino | Chamwino |

**Jedwali Na. 2: Orodha ya Kata Zenye Nafasi Wazi**

| Na. | Halmashauri | Kata |
|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ya Jiji la Mbeya | Nonde |
| 2. | Halmashauri ya Mji Njombe | Lugenge |
| 3. | Halmashauri ya Mji Mbulu | Bargish |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Muheza | Makole |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Pangani | Mwera |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | Oldonyosambu |
| 7. | Halmashauri ya Wilaya ya Uyui | Igalula |
| 8. | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba | Shelui |
| 9. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa | Mvumi |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Tarime | Nyarero |
| 11. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe | Ilolangulu |

3. Hivyo, kutokana na uwepo wa nafasi wazi tajwa na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 49(1)(b), (2) na (4), 57(1)(a) na (2) 61(1) na (3) na 68(2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sura ya 343, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu ratiba ya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara kama ifuatavyo:

   i. Fomu za uteuzi kwa wagombea wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara zitatolewa kuanzia **tarehe 07 Oktoba, 2026 hadi tarehe 13 Oktoba, 2026;**

   ii. Uteuzi wa wagombea wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara utafanyika **tarehe 13 Oktoba, 2026**;

   iii. Kampeni za uchaguzi wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara zitafanyika kuanzia **tarehe 14 Oktoba, 2026 hadi tarehe 03 Novemba, 2026**; na

iv. Uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara utafanyika siku ya Jumatano **tarehe 04 Novemba, 2026**.

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na Maelekezo ya Tume katika kufanikisha ratiba ya uchaguzi husika.

Imetolewa na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**